



# PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA

P.O. Box 55666  
Dar-es-Salaam, Tanzania.

Tel:  
+255 754 942 678

Email  
info@pst.or.tz

Kumb Na AGM/RUH/2022/02

26 Agosti, 2022

Anayehusika, Salaam.

**YAH: RUHUSA KWA WATAALAMU WA FAMASI KUHUDHURIA KONGAMANO LA SAYANSI NA MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA WAFAMASIA TANZANIA, UTAKAOFANYIKA TAREHE 23-25 NOVEMBA 2022 KATIKA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE- DODOMA**

Rejea Kichwa cha habari hapo juu,

Chama Cha Wafamasia Tanzania, (*Tanzania Pharmaceutical Society PST*), ni taasisi iliyoanzishwa kwa lengo la kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali ili kuwaleta pamoja wanataaluma wa kada ya Famasi na kuendeleza taaluma, kuchochea maadili bora ya utendaji kazi, kutoa mafunzo endelevu na kuchangia kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza. Chama hiki kinatekeleza wajibu wake kwa kuzingatia misingi ya sheria inayosimamia vyama vya kitaaluma, sheria ya Famasi na nyinginezo. Kwa mujibu wa katiba ya PST, pharmacists, pharmaceutical technicians na pharmaceutical assistants wanahusika na kongamano hili.

PST imeshirikiana na Kitengo cha Dawa Wizara ya Afya(PSU), Baraza la Famasi(PC), Mamlaka ya Dawa na vifaa tiba(TMDA), Bohari ya dawa(MSD), OR-TAMISEMI na wadau wengine kuandaa Kongamano la Sayansi kwa wataalamu wa kada ya famasi na wadau wa huduma za kifamasia nchini. Kongamano hili litafanyika tarehe 23 – 25 Novemba, 2022, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodomaya. Kutakua na mada mtambuka kwa wataalamu wote wa kada ya famasi katika suala la ubora wa huduma, maadili, mbinu bora za usimamizi wa dawa na vifaa tiba, kuwafahamisha/kuwakumbusha juu ya sheria, kanuni na miongozi ya kada ya famasi, ambapo tumemuomba **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuwa Mgeni Rasmi atakayetufungulia kongamano hili (**tunasubiri uthibitisho**). Tunatarajia kongamano hili kutumika kufikisha ujumbe mahususi kwa wataalamu wa kada ya famasi na wadau wake wote kwa mustakabali wa taifa.

Ili kufanikisha kongamano hili muhimu, tunachukua nafasi hii kuomba ushirikiano wa hali na mali wa taasisi yako ikiwemo kuwafahamisha, kuwaruhusu na kuwahimiza wanataaluma wote wa kada ya Famasi katika taasisi yako kuhudhuria kongamano hili.

Aidha kila mwanataaluma anatakiwa kulipia Ada ya kongamano na Ada ya chama ya mwaka 2022 kama ifuatavyo, Ada hii haihusishi gharama za usafiri na malazi.

Kundi	Ada ya Kongamano	Ada ya Mwaka 2022	Jumla
Mfamasia	50,000/=	50,000/=	100,000/=
Fundi Dawa Sanifu/Wasaidizi	30,000/=	50,000/=	80,000/=
Wanafunzi	30,000/=	N/A	30,000/=

Ni vema kujiandikisha na malipo haya yakafanyika kwa wakati ili kuruhusu maandalizi mazuri kwa kuzingatia uzito wa kongamano hili.

## EXECUTIVE

**President**  
Fadhili Hezekiah.

**Vice President**  
Mtani Njegere.

**Honorary Secretary**  
Benson Katundu.

**Deputy Secretary**  
Modekai William.

**Treasurer**  
Jeanette Senkondo.



# PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA



**P.O. Box 55666**  
Dar-es-Salaam, Tanzania.



**Tel: +255 754 942 678**



**Email: info@pst.or.tz**

Malipo yote yafanyike katika akaunti ya chama kama ilivyobainishwa hapa chini:

**Jina la Akaunti: The Pharmaceutical Society of Tanzania**  
**Namba ya Account: 23910001642**  
**Benki: National Microfinance Bank – Oyster Plaza Branch**

Kwa taarifa, uthibitisho wa malipo na maulizo tafadhali wasiliana na mwenyekiti wa kamati ya maandalizi kwa namba 0767 991 213 a barua pepe [president@pst.or.tz](mailto:president@pst.or.tz)

Wako katika uboreshaji huduma za kifamasia.

Fadhili Hezekiah  
Rais PST

## EXECUTIVE

**President**  
Fadhili Hezekiah.

**Vice President**  
Mtani Njegere.

**Honorary Secretary**  
Benson Katundu.

**Deputy Secretary**  
Modekai William.

**Treasurer**  
Jeanette Senkondo.